



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UTEKELEZAJI WA MFUMO WA TIKETI MTANDAO HADI 17.08.2022

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inapenda kuwajulisha wasafiri wanaotumia mabasi ya endayo mikoani na nchi jirani na Umma kwa ujumla kwamba imetekeleza maboresho ya mfumo wa Tiketi Mtandao kwa kushirikiana na wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Kumbukumbu Kimtandao (NIDC), Watoa Huduma za Tiketi za Kielektroniki na wadau wengine wa Serikalini na sekta binafsi.

Mamlaka kwa kushirikiana na wadau hao, walifanya kazi ya kuainisha changamoto zilizojitokeza katika mfumo, na baada ya kujiridhisha, wadau wote walikubaliana kutoa muda wa mfumo wa Tiketi Mtandao kufanya kazi kwa majaribio kabla ya kuanza rasmi.

Kipindi cha majaribio kilikua kuanzia tarehe mosi Aprili, 2022 hadi tarehe 30 Juni, 2022. Tarehe mosi Julai, Mamlaka ilitoa muda wa nyongeza wa miezi miwili hadi tarehe 31 Agosti, 2022, ulioambatana na kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa wasafirishaji waliokuwa na changamoto tofauti tofauti ili kuhakikisha mabasi yote yaunganishwe kwenye mfumo huo.

Hadi jana tarehe 17, Agosti, 2022, Jumla ya mabasi 7,649 yamesahiliwa kwenye VTS ambapo 3,916 ziko hai (active) na nyingine 3,733 ama zimetoka kwenye biashara hii au zimekwisha muda wa kutumika.

Hivyo, jumla ya mabasi 2,033 yanayomilikiwa na kampuni 308 za usafirishaji abiria yameshaunganishwa na mfumo wa Tiketi Mtandao kupitia watoa huduma(vendors) wa tiketi hizo. Jedwali Na. 1 linaonesha idadi ya mabasi hai na yaliyounganishwa kwenye tiketi mtandao:

Jedwali Na. 1: Idadi ya mabasi hai na yaliyounganishwa kwenye tiketi mtandao

Maelezo	17.08.2022	31.07.2022
Mabasi Hai kwenye Mfumo (VTS)	3,916	3,912
Yaliyounganishwa	2,033	1,432
Yaliyobaki	1,883	2,480
Asilimia ya Mafanikio	52%	37%

Orodha ya Mabasi yaliyojiunga ipo kwenye Kiambatisho Na. 1.

Pamoja na hatua hii iliyofikiwa, Mamlaka imetoa hadi tarehe 29 Agosti, 2022 watoa huduma (vendors) wa tiketi mtandao wawe wamejiunga kwenye mfumo mkuu unaopitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Katika hatua nyingine, Mamlaka imepanga kuanza kuchukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu ya faini na/au kusitisha huduma ya mabasi yote ambayo yatashindwa kutimiza takwa hili la kisheria ifikapo tarehe 1 Septemba, 2022.

Hivyo, tunawakumbusha wamiliki wa mabasi yote ya abiria yaendayo mikoani na nchi jirani kuhakikisha mabasi yao yote yanajiunga nan a mfumo wa tiketi mtandao kabla ya tarehe 31 Agosti 2022 kwa kuwa baada ya tarehe hiyo hatutaruhusu basi lisilotoa tiketi mtandao kufanya safari.

Aidha, tunawashauri abiria wote wapange safari zao mapema ili kuhakikisha wanakuwa na tiketi mtandao kabla na sio tiketi nyingine kwa kuwa tukizuia basi lisilotoa tiketi mtandao kuanzia tarehe 1 Septemba isilete usumbufu.

Mamlaka inawapongeza wasafirishaji na wadau wote walioshiriki kutimiza takwa la kisheria la mabasi husika kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao.

Tunawakumbusha wamiliki wa mabasi kuhakikisha kuwa tiketi inataarifa zote muhimu, ikiwemo: **Jina la abiria, namba ya basi, tarehe na muda wa safari, kituo cha kuanzia na kumaliza safari, nauli iliyolipwa, anwani na namba za simu za msafirishaji na namba ya tiketi husika.**



Aidha LATRA inawashauri abiria kutumia huduma za mabasi yanayotumia mfumo wa Tiketi Mtandao kwani mfumo huo una faida nyingi kwa abiria, wasafirishaji na Serikali. Pia abiria atumiapo mabasi yanayotumia mfumo wa Tiketi Mtandao ataepuka usumbufu pale ambapo mabasi yasiyotoa tiketi hizo zitakapozuiliwa kutoa huduma.

Ili kuwarahisishia abiria kuyatambua mabasi hayo, Mamlaka itachapisha orodha ya kampuni zinazotumia Tiketi Mtandao katika tovuti ya Mamlaka na kurasa zake za mitandao ya kijamii.

Asanteni kwa kunisikiliza

CPA Habibu J. S. Suluo
MKURUGENZI MKUU
18 Agosti, 2022

